

Maandishi ya Maswali Yanayoulizwa Sana kuhusu Chanjo ya COVID-19

Huenda unasikia mambo mengi kuhusu chanjo za COVID-19 hivi sasa. Tungependa kujibu maswali machache kuhusu jinsi chanjo za COVID-19 zinavyotengenezwa.

Chanjo za COVID-19 zinatengenezwaje kwa haraka?

Kawaida, chanjo hujaribiwa ili kuhakikisha kuwa ni salama na inafanya kazi kabla ya kiasi kikubwa cha chanjo kutengenezwa. Kwa sababu ya janga na pesa kutoka kwa serikali ya kitaifa, wanasayansi wanafanya hatua zote kwa wakati mmoja. Ni chanjo ambazo zimejaribiwa tu na kuthibitishwa kuwa salama zitakazotumika.

Chanjo zinajaribiwa vipi?

Kuna chanjo kadhaa tofauti za COVID-19 zinazojaribiwa. Vipimo hivi huitwa majaribio ya kimatibabu. Kila chanjo hufanyiwa zaidi ya jaribio moja. Kwanza, chanjo hujaribiwa katika kikundi kidogo cha watu wa kujitolea, halafu mamia ya watu, kisha maelfu. Watu wa kujitolea katika majaribio ya chanjo ya COVID-19 hutoka jamii na asili mbalimbali. Huu ni mchakato unaotumika pia kujaribu chanjo zingine.

Chanjo zitaidhinishwaje?

Kwa chanjo ambazo zinathibitishwa katika majaribio yote, timu ya wataalam wa matibabu itakagua matokeo ya jaribio na jinsi watu walivyohisi baada ya kupewa chanjo. Ikiwa chanjo inafanya kazi na ni salama, inakubaliwa. Kuna vikundi vingi vya wanasayansi na wataalam ambao wanakagua data ya usalama wa chanjo za COVID-19 na kutoa mapendekezo. Chanjo zilizoidhinishwa tu ndizo zitapeanwa kwa watu.

Ni kina nani watapewa chanjo kwanza?

Kikundi cha kitaifa kinachoishauri CDC hukagua data na kutoa mapendekezo ya watu wanaopaswa kupewa chanjo kwanza. Baadhi ya vikundi vilivyo katika hatari kubwa ya kuambukizwa COVID-19 au vinavyoweza kuugua sana kutokana na COVID-19 vitapewa chanjo kwanza. Jimbo la Minnesota lina timu ya wataalam ambao watasaidia kuhakikisha kila mtu ana fursa sawa ya kupewa chanjo, likizingatia usawa wa kiafya.

Kadri chanjo zaidi zitakapopatikana, watu wengi wataweza kuchanjwa, lakini itachukua miezi kadhaa kabla ya chanjo inayoweza kumtosha kila mtu ipatikane.

Ili upate maelezo zaidi kuhusu chanjo ya COVID-19, tembelea tovuti ya idara ya afya.

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

09/11/20 (Swahili)

Ili upate maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989.